
JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI (EWURA)**

ewura
Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001: 2015 Certified

# MUHTASARI WA TAARIFA YA UTENDAJI WA SEKTA NDOGO YA UMEME KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24



**MACHI 2025**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI
MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji
ISO 9001: 2015 Certified

# MUHTASARI WA TAARIFA YA UTENDAJI WA SEKTA NDOGO YA UMEME KWA MWAKA WA FEDHA 2023/24

MACHI 2025

# YALIYOMO


UJUMBE WA MWENYEKITI WA BODI ........ iv
DIBAJI ........ v
VIFUPISHO VYA MANENO ........ vi
MUHTASARI WA RIPOTI ........ vii

1.0 UTANGULIZI ........ 1
2.0 MUUNDO WA SEKTA NDOGO YA UMEME ........ 1
3.0 LESENI NA USAJILI ........ 2
4.0 VIBALI VYA UJENZI WA VITUO VYA KUZALISHA ........ 3
5.0 MIKATABA YA KUUZIANA UMEME ........ 3
6.0 BEI ZA KUUZA UMEME ........ 4
7.0 MALALAMIKO NA USULUHISHI ........ 4
8.0 UZALISHAJI WA UMEME ........ 5
8.1 Uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme ........ 5
8.2 Mahitaji ya Umeme ........ 6
8.3 Mgawanyiko Wa Uzalishaji Wa Umeme ........ 7
8.4 Uzalishaji Na Uingizaji Umeme Toka Nchi Jirani ........ 8
8.5 Ushiriki Wa Kampuni Binafsi Kuzalisha Umeme ........ 9
9.0 USAFIRISHAJI UMEME ........ 9
9.1 Miundombinu ........ 9
9.2 Wateja ........ 10
9.3 Ufanisi Wa Miundombinu ........ 10
10.0 USAMBAZAJI UMEME ........ 11
10.1 Miundombinu ........ 11
10.2 Wateja ........ 12
10.3 Ufanisi Wa Miundombinu ........ 12
11.0 UPOTEVU WA UMEME ........ 13
12.0 UWEKEZAJI KWENYE MIUNDOMBINU YA UMEME ........ 14
12.1 Uwekezaji katika miundombinu ya kuzalisha umeme ........ 14
12.2 Uwekezaji Katika Miundombinu ya Kusafirisha Umeme ........ 15
12.3 Ushiriki wa wawakezaji binafsi katika miundombinu ya umeme ........ 16
13.0 NISHATI SAFI YA KUPIKIA ........ 17
14.0 TATHMINI YA USHINDANI KATIKA SOKO ........ 18
15.0 MATOKEO YA UDHIBITI ........ 18

16.0 USIMAMIZI WA MASLAHI YA WATEJA ........ 19
17.0 MUONEKANO WA SEKTA NDOGO YA UMEME KATIKA MIAKA IJAYO .... 20
18.0 MAFANIKIO ........ 21
19.0 CHANGAMOTO ........ 23

# UJUMBE WA MWENYEKITI WA BODI

Kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ninayo furaha kuwasilisha Taarifa ya Utendaji wa sekta ndogo ya umeme kwa Mwaka wa Fedha 2023/24.

Ikumbukwe kuwa miongoni wa malengo ya kimkakati ya EWURA ni kuhakikisha upatikanaji wa uhakika wa umeme na wenye bei nafuu. Hii ni kutokana na ukweli kwamba umeme ni miongoni mwa vichocheo vikuu vya maendeleo ya nchi, uchumi wa viwanda na nishati safi ya kupikia.

Katika mwaka 2023/2024, sekta ndogo ya umeme ilipata mafanikio mbalimbali. Miongoni mwa mafanikio hayo ni kuongezeka kwa wateja, miundombinu, uwekezaji, ufanisi wa utendaji wa kampuni zinazodhibitiwa, na uhakika wa kupatikana umeme.

EWURA inaipongeza serikali kwa uwekezaji katika sekta ndogo ya umeme, ukiwemo mradi wa kuzalisha umeme wa megawati 2,115 wa bwawa la Julius Nyerere. EWURA inaipongeza pia sekta binafsi kwa uwekezaji. Juhudi hizi zimechangia kuhakikisha upatikanaji wa umeme na maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini.

Kwa unyeyekevu mkubwa, nawashukuru viongozi wa Wizara ya Nishati na Wizara ya Maji, kwa miongozo mbalimbali waliotupa. Nawashukuru pia wadau wengine katika sekta ndogo ya umeme kwa ushirikiano wao. Tunawahakikishia kwamba EWURA itaendelea kutoa huduma za kiudhibiti za kiwango cha kimataifa kwa uwazi, uwajibikaji na uhodari.

Mwisho napenda kuipongeza Bodi ya EWURA, Menejimenti na wafanyakazi kwa ushirikiano wao na kuwezesha kukamilika kwa taarifa hii.

Prof. Mark J. Mwandosya
**Mwenyekiti wa Bodi**
Januari, 2025

# DIBAJI

Kwa miaka saba mfululizo, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) imekuwa ikiandaa taarifa za mwaka za utendaji wa taasisi zinazodhibitiwa Tanzania bara. Madhumuni ya taarifa hizo ni kuujulisha umma kuhusu hatua zilizofikiwa na taasisi hizo katika kutoa huduma ya umeme, kupima jitihada za taasisi hizo katika kufikia malengo yao na kupendekeza hatua za kuboresha utoaji wa huduma.

Taarifa hii inajumuisha utendaji wa TANESCO ambayo inazalisha, inasafirisha na kusambaza umeme, pamoja na kuendesha mfumo wa Gridi ya Taifa, na biashara ya umeme nje ya mipaka ya nchi. Pia inahusisha kampuni 27 zenye leseni ya kuzalisha umeme na moja yenye leseni ya usambazaji umeme. Inahusisha pia taasisi 13 zenye usajili wa kuzalisha au kusambaza umeme chini ya megawati moja hasa katika maeneo ambayo hayajafikiwa na gridi ya taifa. Taarifa pia inaeleza faida za utendaji wa leseni 9,059 za wafungaji wa mifumo ya umeme.

Kwa ujumla, utendaji wa taasisi zinazodhibitiwa unaendelea kuimarika na hivyo kuchangia katika mafanikio ya ukuaji wa sekta ndogo ya umeme. Mafanikio hayo ni pamoja na kuongezeka kwa uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme (26.2%), idadi ya wateja waliounganishiwa umeme (14.5%), mahitaji ya umeme (12%), na uzalishaji wa umeme (12.2%).

Mafanikio mengine ni kuongezeka kwa miundombinu ya kusafirisha umeme (9.84%), vituo vya kupooza umeme katika gridi ya taifa (0.98%), miundombinu ya usambazaji umeme (14.5%), na elimu kwa umma juu ya matumizi ya umeme kama nishati safi ya kupikia. Pia kuna mafanikio katika kupungua kwa ukatikaji umeme kwa mteja (48%), kupungua kwa masaa ya mteja kukosa umeme (64%), na upotevu wa umeme (0.04%). Vile vile, mikataba ya utendaji ilisainiwa ili kuhakikisha ufanisi katika utoaji huduma.

Uwekezaji pia umeongezeka, ambapo miradi mbalimbali ipo katika hatua za kukamilika. Uwekezaji huo unahusisha miradi inayojengwa na serikali ikiwemo miradi miwili kuzalisha umeme wa jumla ya megawati 2,235.5 ikiwemo bwawa la Julius Nyerere, miradi 27 yenye kilomita 5,033 za miundombinu ya kusafirisha umeme, na miradi 39 ya vituo vya kupozea umeme. Uwekezaji kutokana na sekta binafsi nao uliongezeka, kwa miradi 39 ya kuzalisha umeme wa megawati 179.6 na ambayo ilikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mafanikio haya yasingewezekana bila ushirikiano mkubwa kutoka serikalini, na hasa Wizara ya Nishati, TANESCO, taasisi zinazodhibitiwa, wadau wa maendeleo, na wadau wengine wote kwa ujumla. Ni matumaini yangu kuwa muhtasari huu utatoa taarifa muhimu kwa wadau kuhusu maendelea ya sekta ndogo ya umeme nchini.

Dkt. James A. Mwainyekule
**Mkurugenzi Mkuu**
Januari, 2025

# VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| EWURA | Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji |
| TANESCO | Shirika la Umeme Tanzania |

# MUHTASARI WA RIPOTI

Ripoti hii inawasilisha utendaji wa kiudhibiti katika sekta ndogo ya umeme kuanzia tarehe 1 Julai 2023 hadi tarehe 30 Juni 2024. Imeandaliwa chini ya Kifungu Na. 30(7) cha sheria ya umeme sura ya 131 kinachoitaka EWURA kutoa taarifa za kiudhibiti zikiwemo zile zinazohusu utendaji wa kampuni zinazodhibitiwa, upatikanaji wa umeme, uwekezaji, ufanisi wa kiutendaji, maendeleo ya umeme, na huduma kwa wateja.

Sekta ndogo ya Umeme ina taasisi mbalimbali zinazochangia katika ukuaji wake. Miongoni mwazo ni Wizara ya Nishati ambayo ndio msimamizi mkuu, EWURA ambayo ina jukumu la udhibiti wa kiufundi na kiuchumi, Wakala wa Nishati Vijijini ambao una wajibu wa kusambaza umeme vijijini, na TANESCO ambayo ina wajibu wa kuzalisha, kusafirisha, kusambaza, na kufanya biashara ya umeme ndani na nje ya nchi. Pamoja na na wadau hawa, zipo pia kampuni binafsi ambazo zinawajibu wa kuzalisha na kusambaza umeme.

Katika Kipindi cha mwaka wa fedha wa 2023/2024, zilichapishwa kanuni za kusimamia uzalishaji, usafirishaji na usambazaji umeme (The Electricity (Generation Transmission and Distribution Activities) Rules, 2023), na kanuni za usimamizi wa ugavi wa umeme (The Electricity (Supply Services) (Amendments) Rules, 2023).

Leseni 9,059 zillikuwa hai kufikia Juni 2024. Kati ya hizo, leseni 1,572 zilitolewa katika mwaka 2023/2024, zikiwemo leseni tatu (3) za kuzalisha umeme na 1,569 za mifumo ya umeme. Katika kipindi hicho, leseni za kuzalisha umeme zilikuwa 30, huku kampuni zilizosajiliwa kuzalisha umeme zikiwa 13.

TANESCO, ambayo ni kampuni ya umma, ndiyo kampuni pekee iliyokuwa na leseni ya usafirishaji umeme, ikimiliki pia leseni ya kuzalisha, kusambaza, kugawa, na kufanya biashara ya umeme nje ya nchi. Vilevile, iliidhinishwa mikataba minne ya kuanza kwa mchakato wa ujenzi wa vituo vya kuzalisha umeme vyenye uwezo wa megawati 736.

Katika kipindi cha marejeo ya ripoti hii, mikataba 59 ya kuuziana umeme ilikuwa hai, ikiwemo mikataba 27 iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2023/2024. Vilevile, kampuni saba zilikuwa zimeidhinishiwa bei ya kuuza umeme. Katika kipindi hicho, zilitolewa bei za wazalishaji wadogo za kuuza umeme kwenye gridi ya taifa, na malalamiko 146 yaliyohusu TANESCO na wateja wake yalisuluhishwa.

Uwezo wa kuzalisha umeme uliongezeka kwa megawati 500 sawa na asilimia 26.2 kutoka megawati 1,911,46 mwaka 2022/2023 hadi 2,411.33 mwaka 2023/2024. Mahitaji ya umeme yaliongezeka kwa megawati 174.8 sawa na asilimia 12 kutoka 1,470.50 mwaka 2022/2023 hadi megawati 1,645.23 mwaka 2023/2024.

Urefu wa njia za kusafirishia umeme uliongezeka kwa kilometa 674 sawa na asilimia 9.84 kutoka kilometa 6,850 mwaka 2022/2023 hadi kilometa 7,524 mwaka 2023/2024. Vituo vya kupoza umeme viliongezeka viliongezeka vinne, sawa na asilimia 6.4 kutoka 63 mwaka 2022/2023 hadi 67 mwaka 2023/2024. Urefu wa njia za kusambazia umeme uliongezeka kwa kilometa 24,521, sawa na asilimia 15 kutoka 163,744.56 mwaka 2022/2023 hadi 188,266.23 mwaka 2023/2024.

Wateja 559,595 waliongezeka kufikia 4,982,259 mwaka 2023/2024, kutoka wateja 4,422,664 mwaka wa nyuma yake, sawa na asilimia 13. Kukatika kwa umeme kulipungua kwa asilimia 48, kutoka mara 26 mwaka 2022/2023 hadi mara 14 mwaka 2023/2024. Pia muda wa ukatikaji umeme ulipungua kwa asilimia 64 kutoka dakika 1,536 za mwaka 2022/2023 hadi 554 mwaka 2023/2024.

Uwekezaji kwenye miundombinu ya umeme uliongezeka. Serikali iliwekeza kwenye miradi minne ya uzalishaji ya megawati 2,235.5, miradi 27 ya njia za usafirishaji umeme zenye urefu wa kilometa 5,033, na vituo 39 vya kupoozea umeme vyenye uwezo wa MVA 3,801. Sekta binafsi pia iliwekeza kwenye miradi 39 yenye uwezo wa kuzalisha megawati 178.

Uhamasishaji wa matumizi nishati safi ya kupikia uliongezeka, ili kuhakikisha asilimia 80 ya kaya zote nchini zinatumia nishati safi ikiwemo umeme kufikia mwaka 2034, na ushindani wa soko ulionyesha mahitaji ya ushiriki zaidi wa sekta binafsi ambapo TANESCO ilimiliki asilimia 91 ya uzalishaji umeme na sekta binafsi asilimia tisa.

Miongoni mwa changamoto katika kipindi hicho ni ukame ulioathiri mabwawa ya kuzalisha umeme, kuongezeka kwa matumizi ya umeme kutokana na kuanza kwa treni ya umeme kuongezeka kwa magari ya umeme na uhitaji zaidi wa wawekezaji binafsi. Serikali ilizikabili changamoto hizo kwa kuongeza uzalishaji wa umeme kupitia mradi wa bwawa la umeme la Julius Nyerere.

Kwa ujumla, sekta ndogo ya umeme iliendelea kuimarika. Serikali kwa kushirikiana na wadau itaendelea kuwekeza na kuweka mazingira mazuri kwa wawekezaji binafsi ili kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika na huduma bora kwa wateja.

## 1.0 UTANGULIZI


Nishati ya umeme ni kichocheo muhimu katika ustawi wa maendeleo ya jamii na uchumi. Ni kwa sababu hiyo, serikali imeanzisha taasisi mbalimbali kuhakikisha upatikanaji wa umeme kwa viwango vinavyokubalika kwa mujibu wa sheria na miongozo mbalimbali ya nchi.

Miongoni mwa taasisi muhimu katika sekta hiyo ni pamoja na Wizara ya Nishati ambayo ndio msimamizi mkuu, Wakala ya Nishati Vijijini (REA), Shirika la Ugavi wa Umeme (TANESCO), EWURA ambayo inadhibiti kiufudi na kiuchumi, na wawakezaji binafsi ambao pia wanatoa huduma za umeme.

Ripoti hii inatoa taarifa ya utendaji katika sekta ndogo ya umeme kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa taasisi zinazotoa huduma ya umeme nchini. Huduma hizo ni pamoja na uzalishaji, usafirishaji, usambazaji, na biashara ya umeme nje ya mipaka ya nchi. Ripoti hii imeandaliwa kwa mujibu wa kifungu cha 30 cha sheria umeme sura 131 ambacho kinaitaka EWURA kufuatilia, kupima na kutoa taarifa kwa umma juu ya utendaji wa taasisi zinazodhibitiwa. Vyanzo vya taarifa zilizotumika katika uandaaji wa ripoti hii ni taasisi husika, na kaguzi mbalimbali za EWURA katika taasisi hizo.

## 2.0 MUUNDO WA SEKTA NDOGO YA UMEME

Sekta ndogo ya umeme inahusisha taasisi mbalimbali kama zilivyoainishwa kwenye **Kielelezo Na. 1**. Vilevile, kuna nyenzo mbalimbali zinazosaidia katika uendeshaji na usimamizi, zikiwemo sera, sheria, miongozo, mipango, mikakati, mikataba ya utendaji, na viwango vya ubora.




**Kielelezo Na. 1: Taasisi Muhimu Katika Sekta Ndogo ya Umeme**

## 3.0 LESENI NA USAJILI

Huduma za umeme zinazoanzia megawati moja (1) na zaidi, zinahitaji kuwa na leseni kwa mujibu wa kifungu Na.8(10 cha sheria ya umeme sura 131. Pia huduma zilizo chini ya megawati moja zinahitaji kusajiliwa kwa mujibu wa kifungu namba 18(3).Hadi kufikia Juni 2024, kulikuwa na leseni 9,059 zilizotolewa (**Kielelezo Na. 2**). Kati ya hizo, leseni 1,572 zilitolewa kwa mwaka wa fedha 2023/2024. Pia kampuni 13 zilisajiliwa.




**Kielelezo Na. 2: Leseni Zilizotolewa Kufika Juni 2024**

## 4.0 VIBALI VYA UJENZI WA VITUO VYA KUZALISHA

Kufikia Juni 2024, miradi minne ilikuwa imepata vibali vya ujenzi wa vituo vya kuzalishia umeme kwa mujibu wa kifungu cha 5(d) cha sheria ya umeme sura ya 131. Mchanganuo wa miradi hiyo uko kwenye **Kielelezo Na. 3**.




**Kielelezo Na. 3: Ujenzi wa vituo vya kuzalisha umeme kufikia Juni 2024**

## 5.0 MIKATABA YA KUUZIANA UMEME

Kufika Juni 2024, mikataba 59 ya kuuziana umeme wa jumla ya megawati 629.13 ilikuwa imeidhinishwa kwa mujibu wa kifungu cha 25(3) cha sheria ya umeme sura ya 131, (**Kielelezo Na. 4**). Mikataba hiyo ilisainiwa kati ya TANESCO na kampuni binafsi za kuzalisha umeme za ndani na nje ya nchi. Kati ya mikataba hiyo, mikataba 27 ya umeme wa megawati 332 iliidhinishwa mwaka 2023/2024. Katika mikataba mingine 20, ujenzi wa mitambo umekamilika na kuchangia kwa ongezeko la megawati 449 kwenye gridi ya taifa. Mikataba sita yenye uwezo wa megawati 19.13 iko kwenye hatua za ujenzi, na mikataba 33 ya umeme wa megawati 160 iko katika maandalizi ya kuanza ujenzi.




**Kielelezo Na. 4: Mikataba ya Kuuziana Umeme, kufikia Juni 2024**

## 6.0 BEI ZA KUUZA UMEME

Kufikia Juni 2024, bei za umeme ziliidhinishwa kwa makundi mbalimbali ya wazalishaji mujibu wa kifungu cha 5(b) cha sheria ya umeme sura ya 131, (**Kielelezo Na. 5**). Miongoni mwa bei hizo, ni zile za kuuza umeme kwa wateja na ambazo zilitolewa kwa kampuni saba (7) ikiwemo TANESCO na bei za kampuni binafsi kuuza umeme kwa TANESCO kwa mitambo yote yenye uwezo chini ya megawati moja.




**Kielelezo Na. 5: Bei za Kuuza Umeme Kufikia Juni 2024**

## 7.0 MALALAMIKO NA USULUHISHI

Usuluhishi wa malalamiko ya wateja dhidi ya watoa huduma wao ulifanyika kwa mafanikio na kwa mujibu wa sheria, ambapo malamiko 146 kati ya TANESCO na wateja wake yalisuluhishwa (Kielelezo 7) katika kipindi cha mapitio ya ripoti hii (**Kielelezo Na. 6**).





**Kielelezo Na. 6: Usuluhishi wa Malalamiko kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024**

## 8.0 UZALISHAJI WA UMEME

Taarifa za uzalishaji wa umeme huzingatia vigezo mbalimbali, kama vile uwezo wa mitambo, mahitaji ya umeme, mgawanyiko wa uzalishaji wa umeme, uzalishaji na uingizaji umeme toka nchi jirani na ushiriki wa kampuni binafsi.

### 8.1 Uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme

Kufikia Juni 2024, uwezo wa mitambo kuzalisha umeme ulikuwa megawati 2,411 (**Kielelezo Na. 7**), ambapo TANESCO inachangia kwa asilimia 90.8 (**Kielelezo Na.8**).





**Kielelezo Na.  7: Uwezo wa mitambo Kuzalisha Umeme Kufikia Juni 2024**

| Melezo | Kampuni | Uwezo wa Mitambo (Megawati) | Asilimia (%) | Mchango Katika Gridi |
|---|---|---|---|---|
| Gridi Ya Taifa | TANESCO | 2,160.70 | 91.06% | 98.41% |
| | Wazalishaji Binafsi Wakubwa (SONGAS) | 189 | 7.96% | |
| | Wazalishaji Binafsi Wadogo | 23.26 | 0.98% | |
| | **Jumla** | **2,372.96** | **100.00%** | |
| Nje ya Gridi ya Taifa | TANESCO | 28.942 | 75.42% | 1.59% |
| | Wazalishaji Binafsi Wadogo | 7.4 | 19.28% | |
| | Wazalishaji Binafsi Wadogo Zaidi | 2.03 | 5.29% | |
| | **Jumla** | **38.372** | **100.00%** | |
| Jumla Kuu | TANESCO | 2,189.64 | 90.81% | 100.00% |
| | Wazalishaji Binafsi Wakubwa (SONGAS) | 189 | 7.84% | |
| | Wazalishaji Binafsi Wadogo | 30.66 | 1.27% | |
| | Wazalishaji Binafsi Wadogo Zaidi | 2.03 | 0.08% | |
| | **Jumla** | **2,411.33** | **100.00%** | |
| | | | | |

**Kielelezo Na.  8: Mchango katika Mitambo ya Kuzalisha Umeme - Mwaka 2023/2024**

## 8.2 Mahitaji ya Umeme


Mahitaji ya umeme nchini yameendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka kutokana na kukua kwa uchumi na shughuli za maendeleo ya kijamiii. Kufikia Juni 2024, mahitaji ya umeme katika gridi ya taifa yalikuwa yamefikia megawati 1,645.2 (**Kielelezo Na.  9**).




**Kielelezo Na. 9: Mahitaji ya Umeme Kufikia Juni 2024**

## 8.3 Mgawanyiko Wa Uzalishaji Wa Umeme

Uzalishaji wa Umeme katika gridi ya taifa ulichangiwa na mitambo ya gesi, maji, mafuta na tungamo taka. Gesi ilichangia kwa asilimia 67.10, maji kwa asilimia 32.42, mafuta kwa asilimia 0.47, na tungamo taka kwa asilimia 0.01 (**Kielelezo Na. 10**).




| | 2017/18 | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tungamo Taka | 0.23% | 0.20% | 0.20% | 0.18% | 0.00% | 0.12% | 0.01% |
| Mafuta | 3.75% | 0.10% | 0.00% | 0.15% | 0.19% | 0.14% | 0.47% |
| Maji | 31.89% | 32.30% | 37.39% | 39.12% | 31.49% | 26.92% | 32.42% |
| Gesi | 64.11% | 67.50% | 62.41% | 60.55% | 68.32% | 72.82% | 67.10% |

**Kielelezo Na. 10: Mgawanyiko Wa Uzalishaji Umeme Kufikia Juni 2024**

## 8.4 Uzalishaji Na Uingizaji Umeme Toka Nchi Jirani

Kiwango cha uzalishaji umeme nchini na ule wa kutoka nchi za jirani kiliendelea kuongezeka hadi kufikia 11,068.4 GWh kufikia Juni 2024 (**Kielelezo Na. 11**). TANESCO ilichangia asilimia 82.63 ya umeme wote uliozalishwa na ule wa kutoka nchi za jirani (**Kielelezo Na. 12**).




| | Jumla | Gridi ya Taifa | Nje ya Gridi ya Taifa | Kutoka Nchi za Jirani |
|---|---|---|---|---|
| 2017/18 | 7,670.5 | 7,372.9 | 183.9 | 113.7 |
| 2018/19 | 7,590.6 | 7,372.9 | 96.6 | 121.1 |
| 2021/22 | 9,150.3 | 8,912.2 | 87.5 | 150.6 |
| 2019/20 | 7,787.2 | 7,602.5 | 75.1 | 109.6 |
| 2020/21 | 8,177.7 | 7,973.3 | 78.9 | 125.5 |
| 2022/23 | 9,864.8 | 9,606.6 | 84.4 | 173.8 |
| 2023/24 | 11,068.4 | 10,704.5 | 99.7 | 264.3 |


**Kielelezo Na. 11: Uzalishaji wa umeme kufikia Juni 2024**

| Maelezo | Kampuni | Umeme uliozali | Mchango kwa Asilimia |
|---|---|---|---|
| Gridi ya Taifa | TANESCO | 9,063.58 | 84.67% |
| | Wazalishaji Binafsi Wakubwa (Songas) | 1,520.03 | 14.20% |
| | Wazalishaji Binafsi Wadogo | 120.85 | 1.13% |
| | **Jumla Katika Gridi ya Taifa** | **10,704.46** | **100.00%** |
| Nje ya Gridi ya | TANESCO | 81.8 | 82.09% |
| | Wazalishaji Binafsi Wadogo | 13.76 | 13.81% |
| | Wazalishaji binafsi Wadogo Zaidi | 4.09 | 4.10% |
| | **Jumla Nje ya Gridi ya Taifa** | **99.65** | **100.00%** |
| Mchi za Jirani | Kigagati (Uganda) | 37.54 | 14.20% |
| | Kyaka (Uganda) | 116.27 | 43.99% |
| | Mbala (Zambia) | 59.55 | 22.53% |
| | Rusumo Power Company Limited (Rwanda) | 50.93 | 19.27% |
| | **Jumla Kutoka Nchi za Jirani** | **264.29** | **100.00%** |
| Mjumuisho | TANESCO | 9,145.38 | 82.63% |
| | Wazalishaji Binafsi Wakubwa (SONGAS) | 1,520.03 | 13.73% |
| | Wazalishaji Binafsi Wadogo | 134.61 | 1.22% |
| | Wazalishaji binafsi Wadogo Zaidi | 4.09 | 0.04% |
| | Nchi za Jirani | 264.29 | 2.39% |
| | **Jumla Kuu** | **11,068.40** | **100.00%** |
| | | | |

**Kielelezo Na. 12: Mgawanyiko wa Uzalishaji Umeme - 2023/2024**

## 8.5 Ushiriki Wa Kampuni Binafsi Kuzalisha Umeme

Kampuni binafsi zimekuwa na mchango mkubwa katika uzalishaji wa umeme nchini. Kufikia Juni 2024, uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme kutoka kwenye kampuni binafsi ulifikia megawati 221.7 (**Kielelezo Na. 13**)




**Kielelezo Na. 13: Ushiriki wa Kampuni Binafsi Kuzalisha Umeme Kufikia Juni 2024**

# 9.0 USAFIRISHAJI UMEME

Taarifa juu ya usafirishaji wa umeme ilizingatia vigezo mbalimbali. Miongoni mwa vigezo hivyo ni miundombinu husika, ufanisi wake, na wateja.

## 9.1 Miundombinu

Kufikia Juni 2024, urefu wa miundombinu ya njia za kusafirishia umeme ilifikia kilometa 7,524. Vilevile, uwezo wa vituo vya kupoozea umeme ulifikia MVA 6,669 *(***Kielelezo Na. 14***).*




**Kielelezo Na. 14: Uwezo wa Miundombinu ya Njia za Kusafirisha Umeme**

## 9.2 Wateja

Kufikia Juni 2024, wateja wakubwa saba walikuwa wameunganishwa kwenye miundombinu ya usafirishaji (**Kielelezo Na. 15**). Wateja hao wameunganishwa katika msongo wa kilovoti 220 na 132.

| Wateja Walionganishwa Kwenye Miundo Mbinu ya Usafirishaji | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Mgodi wa Dhahabu wa Bulyanhulu ( 220kV) | Shirika la Umeme Zanzibar (132kV) | Kiwanda cha Simenti cha Tanganyika Portland (132kV) | kiwanda cha Simenti cha Tanga (132kV) | Kiwanda cha simenti cha Rhino (132kV) | Mgodi wa Dhahabu wa Nyamongo (132kV) | Mgodi wa Dhahabu wa Buzwagi (132kV) |

**Kielelezo Na. 15: Wateja Kwenye Miundombinu ya Kusafirisha Umeme Kufikia Juni 2024**

## 9.3 Ufanisi Wa Miundombinu

Ufanisi wa miundombinu ya usafirishaji umeme uliendelea kuimarika (**Kielelezo Na. 16**). Kwa mwaka 2023/2024, kiwango cha upatikaji kilikuwa mara 8.1 ambacho ni chini ya kikomo cha mara 10, wakati ambapo masaa ya ukatikaji umeme yalikuwa 6.3, ambayo ni chini ya kikomo cha masaa 6.5.




**Kielelezo Na. 16: Ufanisi wa Miundombinu ya Usafirishaji kufikia Juni 2024**

# 10.0 USAMBAZAJI UMEME

Taarifa juu ya usafirishaji wa umeme ilizingatia vigezo mbalimbali. Miongoni mwa vigezo ni miundombinu, wateja na ufanisi wa miundombinu.

## 10.1 Miundombinu

Miundombinu ya usambazaji wa umeme iliendelea kuongezeka. Kufikia Juni 2024, urefu wa miundombinu hiyo ulifikia kilomita 188,266.23 kwa kampuni zenye leseni (**Kielelezo Na. 17**), na kilometa 617 kwa kampuni zilizosajiliwa (**Kielelezo Na. 18**). Ongezeko hili limewezesha Watanzania wengi zaidi kupata huduma ya umeme.




| | Jumla | TANESCO | Mwenga |
|---|---|---|---|
| 2017/18 | 103,640.36 | 103,289.36 | 351.00 |
| 2018/19 | 109,639.60 | 109,225.60 | 414.00 |
| 2019/20 | 139,529.86 | 139,092.86 | 437.00 |
| 2020/21 | 148,983.23 | 148,544.23 | 439.00 |
| 2021/22 | 160,810.86 | 160,366.86 | 444.00 |
| 2022/23 | 163,744.56 | 163,296.06 | 448.50 |
| 2023/24 | 188,266.23 | 187,817.73 | 448.50 |

**Kielelezo Na. 17: Miundombinu ya kusambaza umeme kwa kampuni zenye leseni**





| | Jumla | Powercorner | Jumeme | PowerGen | EON | Watu na Umeme | Andoya |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2019/20 | 448 | 152.0 | 104.7 | 112.9 | 46.2 | 7.8 | 24.8 |
| 2020/21 | 596 | 152.0 | 215.5 | 150.2 | 46.2 | 7.8 | 24.8 |
| 2021/22 | 597 | 152.0 | 215.5 | 150.2 | 46.2 | 7.8 | 25.00 |
| 2022/23 | 617 | 152.0 | 247.1 | 150.2 | 0.0 | 7.8 | 59.79 |
| 2023/24 | 617 | 152.0 | 247.1 | 150.2 | 0.0 | 7.8 | 59.79 |

**Kielelezo Na. 18: Miundombinu ya Kusambaza Umeme kwa Kampuni Zenye Usajili**

## 10.2 Wateja

Idadi ya wateja waliounganishwa kwenye miundombinu ya kusambaza umeme iliendelea kuongezeka (**Kielelezo Na. 19**). Kufikia Juni 2024, idadi ya wateja ilikuwa 4,992,259. Kati ya hao, TANESCO ina wateja 4,957,278 sawa na asilimia 99.3. Mchanganuo wa idadi ya wateja kwa kampuni ndogo zenye usajili unapatikana kwenye **Kielelezo Na. 20**.




| | Jumla | TANESCO | Mwenga | Kampuni Zenye Usajiri |
|---|---|---|---|---|
| 2017/18 | 24,177,260 | 2,223,638 | 2,921 | 0 |
| 2018/19 | 2,488,158 | 2,484,202 | 3,956 | 0 |
| 2019/20 | 2,880,350 | 2,864,560 | 4,591 | 11,199 |
| 2020/21 | 3,312,574 | 3,290,490 | 5,105 | 16,979 |
| 2021/22 | 3,864,696 | 3,842,096 | 5,621 | 16,979 |
| 2022/23 | 4,422,664 | 4,400,070 | 5,636 | 16,958 |
| 2023/24 | 4,982,259 | 4,957,278 | 7,269 | 17,712 |

**Kielelezo Na. 19: Idadi ya Wateja**




| | Powercorner | PowerGen | Andoya | Watu na Umeme | EON | Jumeme | Total |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2019/20 | 3,011 | 2,177 | - | 256 | 476 | 4,874 | 10,794 |
| 2020/21 | 3,013 | 3,227 | 278 | 256 | 476 | 9,860 | 17,110 |
| 2021/22 | 3,013 | 3,227 | 278 | 256 | 476 | 9,860 | 17,110 |
| 2022/23 | 3,013 | 3,227 | 278 | 256 | - | 10,460 | 17,234 |
| 2023/24 | 3,013 | 3,227 | 278 | 256 | - | 10,938 | 17,712 |

**Kielelezo Na. 20: Idadi ya wateja kwa kampuni ndogo zenye usajili**

## 10.3 Ufanisi wa Miundombinu

Ufanisi wa miundombinu ya usambazaji umeme uliendelea kuimarika. Katika kipindi cha marejeo, wastani wa ukatikaji wa umeme ulikuwa mara 14 ambao ni chini ya kikomo cha mara 26 (**Kielelezo Na. 21**). Wastani wa masaa ya ukatikaji umeme yalikuwa dakika 554 ambayo ni chini ya kikomo cha 1,536 (**Kielelezo Na. 22**).





**Kielelezo Na. 21: Wastani wa idadi ya ukatikaji umeme**




**Kielelezo Na. 22: Wastani wa Dakika za Ukatikaji Umeme**

## 11.0 UPOTEVU WA UMEME

Kiwango cha upotevu wa umeme kiliendelea kupungua katika kipindi cha marejeo (**Kielelezo Na. 23**). Kwa mwaka 2023/2024, upotevu wa umeme katika miundombinu ya kusafirishia ilipungua hadi kufikia asilimia 5.8, wakati ambapo kwa miundombinu ya usambazaji umeme ilikuwa asilimia 8.7.





Kielelezo Na. 23: Upotevu wa Umeme

## 12.0 UWEKEZAJI KWENYE MIUNDOMBINU YA UMEME

Uwekezaji katika sekta ndogo ya umeme uliendelea kuimarika. Miradi mbalimbali ya uzalishaji na usafirishaji umeme iliendelea kutekelezwa, kama inavyoelezwa katika sehemu inayofuata.

### 12.1 Uwekezaji katika miundombinu ya kuzalisha umeme


Serikali inatekeleza miradi minne ya kimkakati ambayo iko katika hatua mbali mbali (**Kielelezo Na.24**). Miradi hiyo ina uwezo wa kuzalisha megawati 2,235.5 pindi itakapokamilika.





Kielelezo Na. 24: Maendeleo ya Miradi ya Kuzalisha Umeme kufikia Juni 2024

## 12.2 Uwekezaji Katika Miundombinu ya Kusafirisha Umeme

Serikali inatekeleza miradi 27 ya njia za kusafirisha umeme zenye urefu wa kilometa 5,033, ikiwa katika hatua mbalimbali (**Kielelezo Na. 25**). Vilevile, miradi 39 ya vituo vya kupooza umeme yenye uwezo wa MVA 3,801 ilikuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji (**Kielelezo Na. 26**).





**Kielelezo Na. 25: Maendeleo ya Miradi ya Njia za Kusafirisha Umeme**




**Kielelezo Na. 26: Maendeleo ya Miradi ya Vituo Vya Kupoza Umeme kufikia Juni 2024**

## 12.3 Ushiriki wa wawakezaji binafsi katika miundombinu ya umeme

Miradi binafsi 39 iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji (**Kielelezo Na. 27**). Miradi hiyo itakuwa na uwezo wa kuzalisha umeme wa megawati 179.6.




**Kielelezo Na. 27: Ushiriki wa Kampuni Binafsi Katika Uwekezaji Hadi Kufikia Juni 2024**

## 13.0 NISHATI SAFI YA KUPIKIA


Mkakati wa Nishati Safi ya Kupikia wa Mwaka 2024 unalenga kuhakikisha kuwa asilimia 80 ya kaya zote nchini zinatumia nishati safi ya kupikia kufikia mwaka 2034. Takwimu zinaonyesha kuwa hadi kufikia mwaka 2021, asilimia 6.9 tu ya kaya ndio zilikuwa zikitumia nishati safi kupikia (**Kielelezo Na. 27**). Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kufikia lengo ikiwemo kuweka mifumo thabiti ya kiudhibiti ya kuvutia matumizi ya nishati safi, upatikanaji wa umeme, upatikanaji wa vifaa nafuu vya kupikia vinavyotumia umeme, na uhamasishaji wa wananchi.




**Kielelezo Na. 28: Kaya Zenye Nishati Safi ya Kupikia Kufika Mwaka 2021**

## 14.0 TATHMINI YA USHINDANI KATIKA SOKO

Ushidani katika soko unaonyesha kuwa TANESCO inamiliki asilimia 91 ya mitambo ya kuzalisha umeme (**Kielelezo Na. 29**). Hii inaonyesha uhitaji mkubwa uliopo wa ongezeko la wawekezaji binafsi.




**Kielelezo Na. 29: Ushindani wa Soko Kwa Umiliki wa Vyanzo vya Kuzalisha Umeme Kufika Mwaka 2021**

## 15.0 MATOKEO YA UDHIBITI

Udhibiti umechangia sehemu kubwa ya maendeleo ya sekta ya umeme, kiuchumi, na kijamii katika ujumla wake. Miongoni mwa matokeo ya udhibiti ni kama ifuatavyo:

### 1). Uwezo wa Kumudu Gharama za Umeme

- Leseni 1,569 za ufungaji mifumo ya umeme na gharama za mauziano ya umeme ziliidhinishwa mara saba (7) mwaka 2023/2024, na zilichangia kuimarisha ushindani katika soko na kudhibiti bei za umeme, hivyo kusaidia uwepo wa gharama zinazohimilika

### 2). Uhakika wa Upatikanaji Umeme

- Leseni tatu (3) za kuzalisha umeme megawati 14.5 pamoja na mikataba 27 ya kuuziana umeme wa megawati 332 itachangia katika uhakika wa upatikanaji umeme pindi itakapokamilika

### 3). Uhakika na Ubora wa Umeme

- Uwepo wa makubaliano ya mikataba ya utendaji pamoja na ukaguzi wa mara kwa mara kwa kampuni zinazodhibitiwa, umechangia kuimarika kwa uhakika na ubora wa umeme unaopatikana kwa asilimia 48.

### 4). Uwekezaji

- Mazingira mazuri ya uwekezaji pamoja na mifumo mizuri ya kiudhibiti, yamechangia serikali kuwekeza katika miradi minne ya kuzalisha umeme (megawati 2,235.5), miradi 27 ya njia za kusafirisha umeme (kilometa 5,033), vituo 39 vya kupoza umeme (MVA 3,801) na uwekezaji wa kampuni binafsi katika miradi 39 ya kuzalisha umeme wa megawati 179.59.

### 5). Ustawi wa Kampuni Zinazodhibitiwa

- Uidhinishwaji mara saba (7) wa gharama za umeme na mikataba 27 ya mauziano ya umeme imechangia kuhakikisha mapato stahiki kwa uwekezaji na hivyo kuchangia kustawi kwa kampuni hizo.

### 6). Usambazaji Umeme

- Mafanikio yaliyopatikana katika kuidhinisha leseni, bei za umeme, na mikataba ya mauziano ya umeme, yalichangia kuunganishwa umeme kwa wateja wapya 554,867.

## 16.0 USIMAMIZI WA MASLAHI YA WATEJA

Katika kusimamia maslahi ya wateja wa huduma zinazodhibitiwa, hatua mbalimbali zilichukuliwa. Miongoni mwa hatua hizo ni:

### 1). Mkataba wa Huduma kwa Wateja

- Ukaguzi wa mara kwa mara ulifanyika kwa kampuni zote zinazodhibitiwa iii kuhakikisha kuwa zinatii makubaliano yaliyomo kwenye mikataba ya huduma kwa wateja. Hii ilisaidia utendaji kufika asilimia 82 na hivyo kuchangia katika kuimarika kwa huduma kwa wateja.

### 2). Ukaguzi wa Utendaji

- Ukaguzi wa mara kwa mara ulifanyika kwa kampuni zote zinazodhibitiwa iii kuhakikisha kuwa zinatii miongozo ya kisheria na taratibu mbalimbali za kiudhibiti katika utoaji wa huduma kwa wateja. Ukaguzi ulifanyika katika mikoa yote nchini na kwa kampuni zote zinazodhibitiwa.

### 3). Mikataba ya Utendaji

- Mkataba wa utendaji ulisainiwa baina ya EWURA na TANESCO tarehe 14 Juni 2024 ili kuhakikisha kuwa utendaji unakidhi viwango vilivyokubalika katika kutoa huduma kwa mteja. Mikataba kama hiyo itaingiwa na kampuni zote zinazodhibitiwa katika mwaka wa fedha 2024/2025.

## 17.0 MUONEKANO WA SEKTA NDOGO YA UMEIV1E KATIKA MIAKA IJAYO

Sekta ndogo ya umeme inaendelea kukua kutokana na kuwa na mchango mkubwa kiuchumi na kijamii. Muonekano wa sekta ndogo ya umeme katika miaka ijayo unatarajiwa kuwa kama ifuatavyo:

### 1). Mahitaji ya Umeme

- Mahitaji ya umeme yanakadiriwa kuendelea kukua kwa asilimia 11.7% kwa mwaka. Ukuaji huo unakadiriwa kuongeza mahitaji ya umeme hadi megawati 2,677 katika mwaka wa 2025, megawati 4,878 (2030), Megawati 8,554 (2035), megawati 12,854 (2040), na megawati 17,611 (2044).

### 2). Uzalishaji Umeme

- Kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya umeme, uzalishaji wake unatarajiwa kuongezeka pia. Uzalishaji unakadiriwa kuwa megawati 2,677 mwaka 2025, megawati 4,878 (2030), megawati 8,554 (2035), megawati 12,854 (2040), na megawati 17,611 (2044).

## 18.0 MAFANIKI0

Sekta ndogo ya umeme imekuwa na mafanikio kadhaa katika mwaka 2023/2024. Miongoni mwa mafanikio hayo ni kama ifuatavyo:

### 1). Leseni za Kuzalisha Umeme

- Leseni tatu (3) za kuzalisha umeme wa megawati 14.5 ziliidhinishwa na zitachangia katika uhakika wa upatikanaji umeme pindi uzalishaji utakapoanza.

### 2). Leseni za Ufungaji Mifumo ya Umeme

- Leseni 1,569 za ufungaji wa mifumo ya umeme zilitolewa kwa watu binafsi iii kuchochea ufungaji bora wa mifumo ya umeme na hivyo kuchangia katika usambazaji wa umeme.

### 3). Mikataba ya Kuuziana Umeme

- Mikataba 27 ya kuuza umeme wa megawati 332 iliidhinishwa. Mikataba hiyo itachangia katika upatikanaji wa umeme wa uhakika pindi itakapokamilika.

### 4). Ukaguzi wa Miundomninu ya Umeme

- Ukaguzi ulifanyika kuhakikisha ufanisi wa utendaji kwa kampuni zote zinazodhibitiwa na kwa mikoa yote nchini. Hii ilichangia katika kuimarika kwa upatikanaji bora wa umeme. Ukaguzi huo ulifanyika kwa kampuni 30 za kuzalisha umeme, kampuni moja ya kusafirisha umeme, na kampuni mbili za kusambaza umeme.

### 5). Ukaguzi wa mikataba ya kuuziana umeme

- Ukaguzi ulifanyika kuhakikisha kuwa mikataba yote ya kuuziana umeme inatekelezwa ipasavyo. Ukaguzi huo ulifanyika kwa mikataba 59 ya uzalishaji umeme wa megawati 629.13.

### 6). Ukaguzi wa Bei za Kuuza Umeme

- Ukaguzi Ulifanyika kuhakikisha kuwa umeme unauzwa kwa wateja kwa mujibu wa bei za umeme zilizoidhinishwa. Hii inahusisha kampuni saba (7) zinazodhibitiwa ikiwemo TANESCO.

## 7). Usuluhishi wa malalamiko

- Malalamiko 146 baina ya wateja na watoa huduma yalisuluhishwa na kufikia muafaka na hivyo kuchangia katika mahusiano mema na kuwalinda wateja na watoa huduma katika haki zao.

## 8). Ongezeko la Uwezo wa Kuzalisha Umeme

- Uwezo wa kuzalisha umeme uliongezeka kwa megawati 499.9 sawa na asilimia 26.15. Ongezeko hilo lilitoka megawati 1,911.46 mwaka 2022/2023 hadi kufika 2,411,33 mwaka 2023/2024.

## 9). Ongezeko la Mahitaji ya Umeme

- Mahitaji ya Umeme yaliongezeka kwa megawati 174.73 sawa na asilimia 11.88. Mahitaji yalitoka megawati 1,470.50 mwaka 2022/2023 hadi 1,645.23 mwaka 2023/2024.

## 10). Ongezeko la Uzalishaji Umeme

- Uzalishaji wa Umeme uliongezeka kwa GWh1,203.63 sawa na asilimia 12.20% kutoka GWh 9,864.77 mwaka 2022/23 kufikia GWh 11,068.40 mwaka 2023/2024.

## 11). Ongezeko la Miundombinu ya Laini ya Usafirishaji Umeme

- Miundombinu ya Usafirishaji Umeme iliongezeka kwa kilometa 674 sawa na asilimia 9.84. Ongezeko lilitoka kilometa 6,850 mwaka 2022/2023 hadi 7,524 mwaka 2023/2024.

## 12). Ongezeko la Vituo vya Kupoza Umeme

- Uzalishaji wa Umeme uliongezeka kwa GWh 1,203.63 sawa na asilimia 12.20% kutoka GWh 9,864.77 mwaka 2022/23 hadi kufikia GWh 11,068.40 mwaka 2023/2024.

## 13). Ongezeko la Miundombinu ya Kusambaza Umeme

- Miundombinu ya usambazaji umeme iliongezeka kwa kilometa 24,521.57 sawa na asilimia 14.98. Ongezeko lilitoka kilometa 163,744.56 mwaka 2022/2023 hadi 188,266.23 mwaka 2023/2024.

### 14). Ongezeko la Wateja wa Umeme

- Wateja waliongezeka kutoka 4,422,664 mwaka 2022/2023 hadi 4,982,259 mwaka 2023/2024. Ongezeko hili ni sawa na wateja 559,595 (asilimia 12.7)

### 15). Kuongezeka kwa Upatikanaji Umem

- Ufanisi katika upatikanaji umeme uliongezeka. Kukatika kwa umeme kulipungua kwa asilimia 48% kutoka mara 26 mwaka 2022/2023 hadi mara 14 mwaka 2023/2024. Pia muda wa kukatika umeme ulipungua kwa asilimia 64 kutoka dakika 1,536 mwaka 2022/2023 hadi dakika 554 mwaka 2023/2024.

### 16). Kuongezeka kwa Uwekezaji

- Uwekezaji uliongezeka katika miundombinu ya umeme. Serikali iliwekeza kwenye miradi minne yenye uwezo wa megawati 2,235.5 ambayo likuwa katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Serikali pia iliwekeza katika miradi 27 ya laini za kusafirisha umeme sawa na kilometa 5,033. Vile vile serikali iliwekeza kwenye vituo vya kupozea umeme 39 vyenye uwezo wa MVA 3,801. Kampuni binafsi ziliwekeza kwenye miradi 39 ya kuzalisha umeme yenye uwezo wa megawati 179.59.

### 17). Uhamasishaji wa Nishati Safi ya Kupikia

- Uhamasishaji wa nishati safi ya kupikia ulifanyika maeneo mbalimbali ya nchi ili kuhakikisha asilimia 80 ya kaya zote nchini zinatumia nishati safi ya kupikia kufika mwaka 2034. EWURA itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kiudhibiti ili kuwezesha kufikia lengo.

## 19.0 CHANGAMOTO

Changamoto kadhaa zilijitokeza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024. Hata hivyo, serikali iliweza kuzitatua kwa kadri zilivyojitokeza. Miongoni mwa changamoto hizo ni kama ifuatavyo:

### 1). Ukame katika Mabwawa ya Kuzalisha Umeme

- Katika Kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024, upungufu wa mvua, uliathiri upatikanaji wa maji ya kutosha katika mabwawa ya kuzalisha umeme. Hata hivyo serikali iliikabili changamoto hiyo kwa kuzalisha umeme kupitia vyanzo mbadala ikiwemo gesi asilia. Vile vile serikali ilijizatiti katika mipango ya muda mrefu kwa kuongeza vyanzo vya uzalishaji umeme kwa nishati mbadala ikiwemo mradi wa kutumia jua wa Shinyanga wenye uwezo wa megawati 50 utakapokamilika.

## 2). Kuongezeka kwa matumizi mapya ya umeme

- Kuongezeka kwa matumizi mapya ya umeme kulichangia kuongezeka kwa mahitaji ya umeme. Miongoni mwa matumizi hayo mapya ni kuanza kwa treni na magari ya umeme, na kupika kwa kutumia umeme. Serikali iliikabili changamoto hiyo kwa kuhakikisha umeme wa kutosha unapatikana kutoka kwenye vyanzo vyote ikiwa ni pamoja na kukamilisha kwa haraka kwa mradi wa kuzalisha umeme wa Bwawa la Julius Nyerere ambalo liliongeza umeme kwenye gridi ya taifa wa megawati 2,115.

## 3). Ushiriki wa Sekta Binafsi

- Mahitaji ya ushiriki wa sekta binafsi yaliendelea kuongeza. Hii ni kutokana na ushiriki wa sekta binafsi kwenye uzalishaji kuwa asilimia 9. Serikali itaendelea kuweka mazingira bora ya kiuwekezaji yakiwemo yale ya kiudhibiti ili kuvutia wawekezaji wengi zaidi.

ewura

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji

ISO 9001 : 2015 Certified

**EWURA Makao Makuu**

Jengo la EWURA, 3 Mtaa wa EWURA, 41104 Tambukareli

S.L.P 2857, Dodoma, Tanzania | **Simu:** +255 26 2 329 002-4

**Nukushi:** +255 26 2329005 | **Barua Pepe:** info@ewura.go.tz

**Tovuti:** www.ewura.go.tz

**Simu ya Bure: 0800110030**

EWURANews EWURATanzania EWURATanzania EWURATV